# Tutakuwa na furaha kama... tutajifunza kujenga amani

"Heri wapatanishi, maana hao wataitwa wana wa Mungu" (Mt 5,9)

## Lengo

Kuhamasisha na kusambaza utamaduni wa amani katika mazingira yetu ya kazi, ili kuwahusisha wengine katika jitihada yetu

## Mambo yaliendaje?

Mwanzoni kuna sehemu ya makaribisho, ambapo inabidi kuacha nafasi ya mazungumzo na mawasilisho ya kile ambacho kila mtu ameishi, mang'a muzi na magumu pia. Kukaribisha maana yake ni kumfanya kila mtu ajisikie nyumbani: ubunifu utatusaidia kupata mbinu zinazofaa. Pia tunaweza kujikumbusha malengo tuliyojiwekea kwenye mkutano wa mwisho: "ulikuwaje?"

## Shughuli ya utambulisho

**MUDA:** kama dakika 30 hivi

**VIFAA:** mabango yenye mambo mawili ya kuigiza ya kuwapa watu walio katika makundi mawili (waigizaji na watazamaji)

**UENDESHAJI:** Shuleni na katika mazingira mengine hutokea wakati mwingine tunataka kueleza kitu kuhusu jitihada yetu ya kujenga amani kwa watu na watoto ambao hawajui Movement, kwa njia ya wazi na rahisi. Zoezi hili linaweza kutusaidia katika hali zinazofanana kupata maneno na motisha zinazofaa.

Tujigawe katika makundi mawili na kufanya igizo: Kundi moja liigize jambo moja, kundi jingine litakuwa watazamaji. Baada ya hapo ni kubadilishana: Kundi lililokuwa la watazamaji litaigiza na lililoigiza litakuwa watazamaji. Tuna dakika 5 za kujiandaa na dakika 10 za kuigiza tukio. Tunawapendekezea hali halisi zifuatazo ...

**Hali halisi ya kwanza:** Run4unity
Kamati ya mtaa wa mji wenu inataka kufanya mpango kuweka pamoja watoto wanaoishi katika eneo hilo. Inaitisha mkutano wa wananchi ambapo vijana pia wanaweza kuwasilisha mapendekezo yao. mnaamua kuwasilisha Run4Unity kama fursa ya kuelimisha watu juu ya amani, na kama mpango ambao unaweza kuivutia jamii hii ya wananchi chipkizi.

*Ni kwa jinsi gani mtawasilisha mada yenu?*

**Watazamaji:** Andaa maswali yenye mvuto na magumu ambayo wananchi watawauliza makutano.

continua »»»»»»»»»»

Hali halisi ya pili: Gazeti la vijana

Katika maktaba ya shule yenu kuna baadhi ya magazeti na majarida ya habari kwa ajili ya utafiti. Makala nyingi zinaripoti za matukio mabaya ambayo husisitiza utamaduni wa "kutokuwa na amani." Inakuja hamu ya kuwasilisha – ili kuomba uanachama – Gazeti la Chipkizi au New City ambayo yanataka kueneza maadili mazuri na kuonesha mchango wa watu wengi katika ujenzi wa amani. Je mnataka kufanya hivyo kwenye mkutano ujao wa shule.

*Mtafanyaje?*

WATAZAMAJI: shirikini kikamilifu kwa maswali ambayo huenda yakaulizwa na wanafunzi wenzenu.

**HITIMISHO:** inawezekana kutoa maoni kwa kikundi kilichofanya uwasilishaji. Kitu gani kilifanikiwa na kilikuwa cha kushawishi hasa? Hata hivyo, je, kuna kitu hakikuwa wazi au chenye ufanisi?
Halafu toa nafasi kwa mazungumzo kati ya wote:

- Matatizo yenu yalikuwa yapi na / au mafanikio yenu? changamoto kubwa ilikuwa ipi? Je mliishinda?
- Kuna kitu muhimu mlichojifunza na mnataka kushirikisha kwenye kikundi?
- Ni nini kilikosekana katika uigizaji? Ni kitu gani mnafanya katika maisha ya kweli ambacho hakikuwa kwenye uigizaji hapa ili kuonesha kujitolea kwenu katika ujenzi wa amani?



## Tuishi hivi

Mimi ni mharabu mkristo, naishi Nchi Takatifu. Mara nyingi nimejikuta katika kizuizi cha Waisrael wakiwachunguza kwa kina watu na viatambulisho. Mahusiano kati ya raia na jeshi ni ya wasiwasi, wakati mwingine chuki husababisha hoja na vurugu. *Uhakika kwamba Mungu anatupenda bila mwisho na huwaita 'wenye heri' waletao amani, ulibadilisha namna yangu ya kukabiliana na udhibiti huo.* Siku moja, zamu yangu ilifika, askari wakanirudisha nyuma, bila sababu, na kunilazimisha nisubiri zamu nyingine. Ilipofika zamu yangu, nilimkabidhi askari hati yangu kwa tabasamu. Yeye, kwa kushangazwa na muonekano wangu, usiokuwa wa kawaida katika mazingira yale, aliniuliza sababu. Nilimwambia kuwa namwamini Mungu na ni Yeye anayenipa furaha. Akifikiri kuhusu mashambulizi mengi yanayosababishwa na vurugu na chuki duniani, aliniuliza kwa nini yule Mungu wangu anaruhusu matukio kama hayo. Nilimweleza kuwa si Yeye anyefanya mambo mabaya, bali ni mwanadamu. Na yeye kwa mshangao : *«Sijawahi kukutana na mtu mwenye furaha hii!»*. Lakini changamoto halisi ilikuwa kujua kwamba hata baadhi ya watoto wa Kiyahudi walitaka, kama sisi, kuishi kwa ajili ya ulimwengu wenye umoja: kama ni kweli kwamba hakuna tofauti kati ya Wakristo, Waislamu na Wayahudi, ilikuwa nimpende kila mtu, bila ubaguzi. Nilipokutana na mmoja wao, Niligundua kwamba, kwa mara ya kwanza katika maisha yangu, nilikuwa nazungumza na Myahudi ambaye hakuwa askari.

> Mara ya kwanza tulikuwa na 'hofu, kidogo kisha kila mmoja alisema alichofikiri juu ya hali halisi: sote wawili tulitaka amani..

*(H. – Terra Santa)*

## Kwa undani

# «NJIA YA AMANI»



***Chiara Lubich,** Castelgandolfo, 6.6.1987*
*Kongamano kuu - n°8*

### Ni njia gani twaweza kuifuata sisi gen 3 ili kujenga amani duniani?

Kwanza kabisa inabidi kuhifadhi amani mioyoni mwenu. Mara nyingi hakuna amani kwa sababu kuna uchungu, mashaka, mahangaiko, kuna kitu kinachotutesa. Hivyo, ili kuwa na amani, inabidi kumkumbatia Yesu mwachika na kutoka "nje" maramoja kuishi nukta ya sasa. Kwa kufanya hivyo amani itarudi.

Halafu inabidi kufanya kila linalowezekana ili tuwe na amani kati yetu, kati ya gen 3 wote duniani. Kama kuna kizuio chochote, kitolewe ili amani iwepo daima, yaani umoja na uwepo wa Yesu kati yetu.

Halafu tuwe na amani na matawi mengine ya Opera kwa kujaribu kuwa na Yesu kati yetu na wote.

Hatimaye ninyi, ili kupeleka amani, mnatakiwa kufufua kila mahali movement ya "Chipkizi wa Umoja" kwa sababu kwa jinsi hii mtatoa hata kwa vijana wengine wengi uwezekano wa kuwa na amani. Hili ndilo jukumu lenu.

# DUNIA INAUELEKEA UMOJA

### Ni mtu gani unadhani anaweza kuwa mfano wa kuigwa na vizazi vijavyo?

Nadhani mtu anayeweza kuwa mfano wa kuigwa na vizazi vijavyo ni mtu wa umoja. Kama tunavyoona sote, sasa katika magazeti na kwenye televisheni, bado kuna vita nyingi, majanga, vitisho vya vita mpya, n.k. Lakini kuna ishara ya nyakati hewani na ishara hiyo ni umoja: dunia, licha ya yote, inauelekea umoja. Nasi tunaona katika mambo mengi: kwa mataifa yanayotaka kuungana, kama Ulaya; kutoka katika Kongamano la Dunia la Dini kwa ajili ya Amani ambalo kwalo dini zinataka kuungana ili kuwa na uwezo wa kuleta amani duniani; kutoka katika makanisa mbalimbali ya Kikristo yanayo uelekea umoja, baada ya karne nyingi ambapo yalikuwa hayaangaliani bali kupigana baina yao. Na kisha tena, kutoka katika taasisi fulani kama vile Umoja wa Mataifa, unaojaribu kuiona dunia kuwa moja au kwa vyombo vya habari vinavyoifanya dunia kuwa nyumba moja.

Mtu wa kesho ni mtu wa umoja, mtu, ambaye sisi tumemwita 'mtu-duniani, mtu anaweza kubeba katika moyo wake hazina zinazotolewa na wengine, kutoka mabara yote, na anayeweza kutoa hazina zake kwa wengine. Mtu wa kesho ni mtu wa umoja, ni mtu-dunia.

***Chiara Lubich,** Palaghiaccio ya Marino (Rm), 10.5.'97 – Kongamano Kuu 3 – n°13*

## Tutajaribu!

- Dunia pamoja na kutamani amani bado inateseka kwa vita nyingi, ambazo hatuzijui kwa sababu hazioneshwi katika vyombo vyetu vya habari. Kwa msaada wa utafiti tunaweka alama juu ya ramani ya dunia, nchi zilizo katika migogoro. Tunaposali TIME-OUT tunaweza kuwaweka mioyoni mwetu wale wote wanaoteseka katika nchi hizi. Kwa njia ya walezi wetu tunaweza kuanzisha mawasiliano na gen 3, au Chipkizi wa umoja wanaoishi katika moja ya nchi hizo.
- Michezo inaweza kuwa nafasi muhimu ya kujenga undugu wa wote, na hasa kama wachezaji ni wa kutoka katika mataifa mengi au wa imani mbali mbali za kidini. Baadhi ya gen3 walitusimulia kuwa waliandaa mashindano au timu ya soka na kuweka SHERIA ZA SPORTS4PEACE. Mwanzoni mwa mchezo na katika wakati maalumu uliopangwa, walirusha dadu na timu licha ya kupata alama za mchezo, walipata pia alama moja kwa kuzingatia hizo sheria sita:

CHEZA KWA BIDII - JITAHIDI! Toa ubora wako, shiriki kwa furaha.
CHEZA KWA HAKI! Uwe mwaminifu kwako mwenyewe na kwa wengine.
NG'ANG'ANA! Usikate tamaa kamwe, hata wakati mambo ni magumu.
WATUNZE! Waheshimu wote: kila mtu ni wa muhimu.
SHEREHEKEA! Furahia ushindi wa wengine kama ushindi wako.
FANYA MABADILIKO! Malengo makubwa hufikiwa pamoja tu.

Ili kujua zaidi fungua ukurasa wa sport4peace:
***http://www.sportmeet.org/eventi/sports4peace/)***



## Tupo katika hatua gani?

*Ili **kulifikia lengo** ni lazima kufanya mazoezi kila siku na kutambua mabadiliko mazuri na magumu yaliyojitokeza. Itatusaidia hadi katika mkutano ujao, tutakapotenga muda wa kushirikishana mang'amuzi.*

Ni kwa jinsi gani tulijitahidi kuwasiliana na kuwashirikisha wengine katika jitihada ya kujenga amani?

Ni nafasi gani zilijitokeza kwangu?

Niliweza kupendekeza nini?

**Kwa ajili ya mlezi**

## Tathmini baada ya mkutano

- Shughuli zilizopendekezwa zilikuza mvuto wa vijana kwa hii heri?
- Kuna eneo la pekee lililojitokeza ambalo gen 3 wanaona kuwa ni vigumu kujenga amani?
- Walichukua dhamira gani ili kuiishi? Lengo liwe kuwaongoza na kuwasaidia katika pendekezo lao hadi mkutano ujao.
- Nafikiri kuwa mada imekamilika au nadhani kuwa kuna kitu kinachokosekana cha kukijadili katika mkutano ujao?
- Kuna magumu yaliyojitokeza? Ni kitu gani cha muhimu kukumbuka ili kuboresha wakati ujao?